KAULI YA ASASI ZINAZOFANYA KAZI NA WAFUGAJI WA ASILI KUHUSU MIGOGORO YA ARDHI TANZANIA

UTANGULIZI:

Ufugaji wa asili

Ufugaji wa asili ni mfumo wa maisha unaohusisha matumizi ya ardhi ambapo wafugaji wanahama kwa mpangilio kutoka eneo moja hadi jingine kwa sababu maalum zikiwemo utafutaji wa malisho, maji na huduma zingine za mifugo baadaye kurudi kwenye maeneo ya awali kwa vipindi maalum.

Kutokana na hali halisi ya upatikanaji wa rasilimali za ufugaji asili nchini na kutofautiana kwa hali ya hewa kutoka eneo moja hadi jingine kwa kipindi cha mwaka, wafugaji wa asili hulazimika kuhama kutoka maeneo wanamoishi na kwenda maeneo mengine na kisha kurejea katika maeneo ya awali kwa vipindi maalum.

Tanzania inashika nafasi ya pili kwa wingi wa mifugo barani Afrika ikiwa na ng'ombe milioni 25, mbuzi milioni 16.7, kondoo milioni 8, nguruwe milioni 2.4, na kuku milioni 36. Kati ya ng'ombe milioni 25 ng'ombe wa asili ni 98%. Hivyo, ni 2% tu ya ng'ombe wote Tanzania wanaofugwa kwa mfumo wa ufugaji wa kisasa, (URT, 2015).

Tafiti zinaonesha kuwa ufugaji wa asili unachangia 7.4% ya pato la Taifa na ongezeko la ukuaji la 2.2% kila mwaka. Ufugaji wa asili umethibitika kiuchumi kuwa na ufanisi mkubwa katika matumizi ya ardhi na uhifadhi wa mazingira. Ufugaji wa asili unategemewa na idadi kubwa ya Watanzania kwa kuendesha maisha yao; iwe kwa chakula, mavazi, na maendeleo kwa mapana yake. Mchango wake katika uchumi rasmi na usio rasmi (informal and formal economies) ni dhahiri hasa kupitia kodi na tozo mbalimbali katika masoko ya mifugo, usafirishaji wa mifugo, ukaguzi wa mifugo, na upatikanaji wa malighafi kwa matumizi ya viwanda mbalimbali.

Tunapongeza kwa dhati kauli za Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alizozitoa wakati wa kampeni na hata baada ya kuingia madarakani zinazoleta matumaini kwa wanyonge walio wengi, hususani wafugaji asilia kutengewa maeneo ya malisho. Tunapongeza pia juhudi za serikali katika kutunga sera na sheria mbalimbali zinazolenga kuboresha maisha ya wafugaji ikiwa ni pamoja na Sera ya mifugo 2006. Tunachukua nafasi hii kupongeza kauli ya Mheshimiwa Wiliam Lukuvi, Waziri wa Ardhi

kama alivyotamka hivi karibuni kutangaza kiama kwa wamiliki wa mashamba yasiyoendelezwa.

MTAZAMO ULIOPO DHIDI YA UFUGAJI WA ASILI

Pamoja na faida hizo zote, bado mfumo huu wa ufugaji asili haujatambulika na kupewa umuhimu wa kutosha katika mfumo wa sera, sheria na mamlaka za kiutawala katika ngazi ya serikali za mitaa na serikali kuu.

Mtazamo hasi wa baadhi ya makundi mbalimbali ya watu katika jamii na hata baadhi ya viongozi wakuu serikalini na wanasiasa dhidi ya ufugaji wa asili, wakichukulia ufugaji asili kama mfumo uliopitwa na wakati, usio na tija na wenye kusababisha uharibifu wa mazingira umepelekea sekta hii kutokupewa umuhimu wake. Kwa mfano, bajeti ndogo isiyotosheleza ya sekta ya mifugo imepelekea kutokuwepo huduma bora za ufugaji wa asili zikiwemo maeneo ya malisho, masoko, miundombinu ya machinjio, majosho, huduma za ugani na mabwawa ya maji. Hali hii imepelekea ufugaji wa asili kukumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo migogoro ya ardhi ambayo imekuwa tishio kwa ustawi wa mfumo huu wa ufugaji asili na jamii kwa ujumla.

VYANZO VYA MIGOGORO

Migogoro ya ardhi ambayo sio tu inawaathiri wafugaji bali na makundi mengine inatokana na sababu mbalimbali zikiwemo:-

- Sheria ya utambuzi wa mifugo 2010 kuzuia uhamaji wa wafugaji wa asili na mifugo yao.
- Sera ya wanyama pori 1998 inazuia uwepo wa mifugo katika maeneo ya wanyama pori ilihali maeneo mengi yanayofaa kwa malisho yakitwaliwa kwa ajili ya uhifadhi.
- Sheria ya hifadhi ya mazingira ya mwaka 2007 inaainisha kuwa ufugaji wa asili ni moja ya vyanzo ya uharibifu wa mazingira jambo linalopotosha jamii na kuleta migongano baina ya wafugaji asili, mamlaka husika na makundi mengineyo **'licha ya ukweli kwamba ufugaji asili ni rafiki wa mazingira'.**
- Migogoro baina ya wakulima na wafugaji asili inatokana na kutokutambulika kwa haki na umiliki wa ardhi ya wafugaji asili.
- Maeneo mengi yaliyokuwa yakitumika na kutambulika kama maeneo ya malisho na njia za mifugo kutowekewa ulinzi wa kisheria kumepelekea uvamizi wa maeneo hayo na makundi mengine ya watu. Aidha, ardhi ya wafugaji imekuwa

ikitambulika kama ardhi isiyotumika (*idle land*), isiyo na mmiliki (unoccupied land) na hivyo kuwa mhanga wa kutwaliwa kwa ajili ya matumizi mengine.

- Mitazamo ya jamii juu ya ufugaji wa asili kuwa wafugaji wa asili ni wavamizi inasababisha chuki inayozaa migogoro isiyokwisha.
- Kutokuheshimiwa kwa mipango halali ya matumizi bora ya ardhi, kutokufuatwa taratibu halali za kupata ardhi, kukosa uadilifu miongoni mwa viongozi wa serikali za mitaa pamoja na kauli za uchonganishi za baadhi ya viongozi wa serikali, kisiasa, mila na dini kwa miaka mingi vimekuwa chanzo cha migogoro ya ardhi. Baadhi ya kauli hizo ni;
    - "mifugo imekonda na wafugaji wamekonda……."
    - "wafugaji warudi huko walipotoka……"
    - "wafugaji hawa ni wavamizi……"
    - ”wafugaji wa asili ni sawa na viwavi jeshi”
    - Na nyingine nyingi.

ATHARI ZA MIGOGORO

Migogoro ya ardhi imepelekea athari mbalimbali zikiwemo vifo vya watu na mifugo, majeruhi na ulemavu wa kudumu, uharibifu wa mali na mazao mashambani, kuzorotesha shughuli za uzalishaji mali kutokana na hofu miongoni mwa wanajamii, umasikini, visasi na chuki miongoni mwa jamii, ubakaji na vitendo vingine vya ukiukwaji wa haki za binadamu pamoja na uharibifu wa makazi. Mifano hai ni Operesheni Tokomeza Ujangili, kufukuzwa wafugaji bonde la Ihefu, Kuchomwa nyumba za wafugaji Loliondo, mapigano na mauaji kati ya wakulima na wafugaji Kiteto na yanayoendelea wilayani Mvomero na Kilosa. Athari nyingine ni hofu inayojijenga miongoni mwa jamii inayowafanya wasijikite katika uzalishaji kwa hofu kwamba wakati wowote vita vitazuka. Hizi ni baadhi tu ya athari nyingi zinazojitokeza.

NINI KIFANYIKE

Kwanza kama taasisi zisizo za kierikali tunachukua hatua hii KULAANI vitendo vya uvinjifu amani, haki za binadamu na za wanyama vilivyojitlokeza wilayani mvomero na kilosa mkaoni morogoro tarehe 14 mwezi huu decemba 2015, vilivopelekea vifo vya watu na mifugo na uharibifu wa mali zao. Kwa kauli moja tunatoa tamko kuitaka seriakli yetu sikivu iwajibike kufanya mabao yafuatayo:-

1. Mheshimiwa waziri wa ardhi kubainisha na kuyaweka wazi maeneo yote ya wafugaji yaliyohodhiwa na wawekezaji rasmi na wasio rasmi ili yarejeshwe kwa wafugaji husika.
2. Serikali kwa kushirikiana na wadau iwe na mkakati wa pamoja wa kuelimisha umma juu ya umuhimu wa amani baina ya makundi yote katika jamii na kulinda haki ya kila mmoja.
3. Serikali iweke mazingira mazuri ya kisera, na ya mgawanyo sawa wa rasilimali yanayoruhusu kila sekta kukua bila kuingiliwa au kuzuiliwa na sekta nyingine.
4. Sheria ya ardhi, wanyama pori na nyingine ziwatambue wafugaji wa asili na mifugo yao kama watanzania wenye uwezo na haki ya kumiliki ardhi.
5. Mifugo itambuliwe rasmi kama rasilimali nyinginezo zinazohitaji kupewa haki ktk umilikaji na matumizi ya ardhi.
6. Serikali iandae sera mahsusi ya ufugaji asili itakayosimamia haki na maendeleo ya sekta hii kwani sera ya mifugo iliyopo haikidhi mahitaji ya ufugaji wa asili.
7. Serikali kupitia Kituo Cha Uwekezaji Tanzania ijiridhishe kiasi cha kutosha kubaini umiliki na matumizi ya maeneo ya ardhi kabla ya kumkabidhi mwekezaji ili kuepusha migogoro baina ya wawekezaji hao na watumiaji wengine wa ardhi.Kwa mfano eneo la utekelzaji wa Kilimo kwanza kupitia mradi au mkakati wa kukuza kilimo ukanda wa kusini "SAGCOT" (Sothern Agricultural Corridor of Tanzania).Mpango wa mkakati huu ni kupata eneo la ardhi kilometa za mraba 300,000 zitakazotoka kwenye ardhi ya kijiji.
8. Serikali kwa kushirikisha wadau ifanye mapitio juu ya sera na sheria zinazogusa masilahi ya wafugaji na wakulima ili kubaini maeneo yanayohitaji maboresho katika utekelezaji kwa ajili ya ukuaji wa mfumo mzima wa uzalishaji mali, ustawi wa amani na mshikamano miongoni mwa makundi yote ya jamii. Utekelezaji wake ufuatene na Serikali kuunda timu itakayojumuisha wataalamu, viongozi wa siasa na wa serikali, asasi za kiraia, wakulima, wafugaji, vyombo vya habari, taasisi za serikali na wawekezaji itakayobaini vyanzo vya migogoro na kupendekeza hatua za kuchukuliwa ili kuondokana na migogoro ya ardhi.

Mwisho: Serikali ihakikishe sheria ichukue mkondo wake bila kuoneana aibu dhidi ya viongozi wote wa serikali, kisiasa, mila na wa dini wanaohusika na kusababisha migogoro ama kwa kupokea rushwa, kutoa kauli za uchochezi, kuzembea katika kusimamia mipango halali ya matumizi bora ya ardhi na kutumia madaraka yao vibaya.

Sambamba na hili tunaitaka serikali ichukue hatua za kisheria dhidi viongozi wa serikali na watendaji husika wilaya za Mvomero, Kilosa na wa mkoa wa Morogoro kwa kushindwa kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji iliyodumu kwa muda mrefu na kusababisha vifo vya watu na mifugo na mali nyingine za jamii.

ORGANIZATION	**LOCATION**
TPCF	Arusha
EKWET	Arusha
SHDEPHA	Kahama
PAICODEO	Kilosa
PINGOs	Arusha
HUDESA	Kilosa
LCDO	Longido
PWC	Ngorongoro
MONDULI WOMEN	Monduli
HADZABE	Mbulu
KITUMUSOTE	Arusha
UNGO	Ngorongoro
CEDESOTA	Arusha
KINNAPA	Kiteto
NAADUTARO	Kiteto
WODSTA	Arusha
TNRF	Arusha
UMWEMA	Morogoro
SWEET	Kiteto
BABATI	Babati
KITETO	Kiteto
TCRIP	Dar Es Salaam
CCWT - Katibu	Dar Es Salaam
M/kiti CCWT TZ	Dar Es Salaam
KITETO	
PAWAGA	Iringa
TANIPE	Kilosa
RIRA	Busega
MMC	Dodoma
BAENET	Dodoma

UWAKAMA	Chimala -Mbeya
HOSF	Hanang
GET	Hanang
SIRUNGONET	Singida
MPF	Monduli
MPDO-LARETO	Monduli
UVIMASHA	Mererani-Arusha
PUFDIA	Same
SHIMWAJAWA	Serengeti
KANDA YA ZIWA	Serengeti
MWEDO	Arusha
TAPHGO	Arusha